



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA FEDHA  
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

Arusha, 30 Aprili, 2024

**WAKULIMA WA TUMBAKU TABORA WALIPWA MAFAO YA FIDIA YA BIMA YA  
KILIMO KUTOKA KAMPUNI YA UAP**

Wakulima wa zao la Tumbaku wa Chama cha Msingi cha wakulima cha *Mtapenda Amcos* chenye namba ya **Usajili 859** wamelipwa mafao ya fidia ya bima ya kilimo na Kampuni ya bima ya UAP kufuatia janga la mvua ya mawe lililowakumba wakulima hao.

Akitoa shukrani zake kwa Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware kuitia barua iliyowasilishwa TIRA, Mkt. wa Chama cha Ushirika cha *Mtapenda Amcos* amesema malipo hayo yamewaimarisha kiuchumi na amewashukuru TIRA na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora kwa ushirikiano na hatimae kufanikisha malipo hayo kwa haraka.

Mnamo Machi 2, 2023 wakulima wa zao la tumbaku mkoani Tabora walikumbwa na janga la mvua ya mawe iliyopelekea uharibifu wa zao hilo na wahusika kuwasilisha madai yao kwenye Kampuni ya bima ya UAP na baadae kulipwa fidia ya Tzs. Mil 374 kuitia Benki ya **NMB**.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania inaendelea kutoa rai kwa watanzania kuwa na utamaduni wa kukata bima mbalimbali zikiwemo bima za kilimo au mali ili kuhakikisha kuwa wanakingwa na majanga pale yanapotokea na hivyo kuwarejesha katika hali zao za kawaida kama ilivyokuwa awali.

**TIRA-Kwa Soko Salama la Bima**

**Hadija I. Maulid**

**MENEJA UHUSIANO NA MAWASILIANO (TIRA)**